**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

**SHULE YA SEKONDARI CHIEF SAROTA**

**S.L.P 148 Mugumu- Serengeti.**

**Mawasiliano**

Mkuu wa shule +255687513745/+255759083706.

Makamu mkuu wa shule: +255689175705/+255715367715

Mwandamizi taaluma: +255693373517

E-mail: yohanamussa60@gmail.com

Kumb.Na.CHF/F.V/JNG.VOL 1/2026

Mzazi/Mlezi wa…………………………………………………………..

SLP……………………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHIEF SAROTA, HALMASHAURI YA SERENGETI MKOANI MARA MWAKA …………**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao…………………………………………………….. amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano mwaka……. Katika tahasusi ya CBG katika shule ya sekondari CHIEF SAROTA ambapo atapata elimu hatimaye kulitumikia taifa. Kama Mzazi / Mlezi unapaswa kumuasa mwanao azingatie masomo Pamoja na taratibu zote za shule na kumpa mahitaji yote ya shule ili aweze kufikia lengo la kitaifa. Aidha aelewe kuwa ni miongoni mwa watanzania wachache waliopata fursa hii na anapaswa kuitumia vizuri.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ………… mwanao atatakiwa kuripoti shuleni tarehe …….. Muda wa kuripoti ni kuanzia **saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni kwa siku za kazi tu**. Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni si zaidi **ya wiki mbili (siku 14)** tangu tarehe ya muhula wa kwanza kuanza. Mara mwanafunzi afikapo shuleni aripoti ofisi ya Makamu Mkuu wa shule kwa ajili ya mapokezi na usajili.

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vifaa vifuatavyo,

i. Mahitaji yote yaliyoelekezwa katika fomu hii

ii. Fomu iliyojazwa na daktari katika hospitali ya SERIKALI kuhusu afya ya mwanafunzi (Medical examination form). Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara mwanafunzi atakapo ripoti shuleni.
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal particular form)
iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina Pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.
v. Aje na Ream mbili za karatasi (DOUBLE A) zinatakiwa (2) kwa mwaka
vi. Fomu ya usajiliwa Mzazi/Mlezi /Ndugu wa karibu wa mwanafunzi.
vii. PICHA (PASSPORT SIZE) moja angalau Mzazi/Mlezi atakaeandikishwa kwenye FOMU ya usajili wa Mzazi /Mlezi/Ndugu wa karibu na mwanafunzi.

Barua hii naambatanisha orodha kamili ya vifaa vya lazima mwanafunzi anavyopaswa kuja Pamoja na fomu hii anazotarajiwa kujaza na kuja nazo wakati wa kuripoti shuleni.

ZINGATIA:

HATUPOKEI MWANAFUNZI SIKU NA SAA AMBAZO SIYO ZA KAZI

……………………

MKUU WA SHULE

1. **JINSI YA KUFIKA SHULENI**
    i. Kwa wanaotokea Dar es salaam, Pwani,Morogoro, Mikoa ya kanda ya kati, Kusini, Nyanda za juu kusini, Kigoma na Kagera; baada ya kufika Mwanza wanashauriwa kupanda mabasi stendi ya NYAMHONGORO- MWANZA yanayoelekea MUGUMU kupitia BUNDA na watashukia kituo cha ISSENYE-SENTA NDOGO. Nauli kutoka MWANZA hadi ISSENYE -SENTA NDOGO ni shilingi 15,000/=.
    ii. Kwa wale wanaotoka mikoa ya kaskazini (Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga) wapande mabasi yanayokwenda MUSOMA kupitia Barabara ya NGORONGORO SERENGETI nauli kutoka ARUSHA mjini hadi ISSENYE-SENTA NDOGO ni Tsh 60,000 hadi 65,000/=.
    iii. Kwa wale wanaotoka mkoa wa MARA ( Musoma MC, Musoma Dc, Tarime, Rorya, Bunda mji, Bunda DC na Butiama) wanaweza kupanda magari kutoka katika stendi kuu za mabasi zilizoko maeneo ya kuelekea ISSENYE-MUGUMU kupitia bunda, Musoma ,Tarime au Butiama kupitia Mugeta na kushukia ISSENYE-SENTA NDOGO, nauli ni kati ya Tsh 15,000/= hadi Tsh 20,000/=.
    iv. Kutoka kituo cha ISSENYE -SENTA NDOGO hadi kufika shuleni CHIEF SAROTA mwanafunzi atatakiwa kupanda usafiri wa bodaboda au pikipiki hadi shuleni( Tsh 4000/=)

**KUMBUKA:**

Mwanafunzi anapaswa/ anashauriwa kumwambia/ kumkumbusha Mhudumu wa gari (Dereva au Kondakta) wa gari alilopanda ili amishushie ISSENYE-SENTA NDOGO na baada ya kushuka panda pikipiki (bodaboda) hadi shuleni**.**

2. **ADA NA MICHANGO YA SHULE**

| NA | AINA YA MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65000/= |
| 2. | Taadhari | 5000/= |
| 3. | Nembo | 5000/= |
| 4. | Kitambulisho cha shule | 5000/= |
| | JUMLA | 80,000/= |

Fedha hiyo ilipwe katika akaunti ya shule Na. 0150878989600- CRDB jina la akaunti CHIEF SAROTA SECONDARY SCHOOL na mwanafunzi afike shuleni na original pay slip iliyoandikwa jina sahihi la mwanafunzi

**3. SARE YA DARASANI.**

- ❖ Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu na yasiyobana mwili.
- ❖ Sketi mbili (02) ndefu za dark blue zinazofikia katika kifundo cha mguu kwenye kisigino. Kitambaa Kizito grade 1 isiyopauka
- ❖ Tai moja rangi ya darkblue yenye mistari nyeupe kama inavyoonekana kwenye picha hapo chini
- ❖ Sweta moja rangi ya kijani kibichi lenye mshono au shingo ya "V" na misitari nyeupe shingoni na mikononi
- ❖ Soksi jozi 2 za rangi nyeupe.
- ❖ Viatu vya Ngozi vyeusi vyenye Kamba jozi 2 visiwe na kisigino kirefu wala shingo ndefu.
- ❖ T-shirt ya blue yenye kola na nembo ya shule, huvaliwa siku ya jumatano. Zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 20,000/= (aje nayo mkononi)
- ❖ Mnunulie viatu na nguo za michezo (Track suit) ni lazima kwa kila mwanafunzi kwa sababu ndio sare ya kuvaa siku ya ijumaa iwe rangi ya "dark blue" yenye ufito mweupe.
- ❖ Wanafunzi wenye imani ya kiislamu wataruhusiwa kushona Hijabu inayofanana na sare ya shule (iwe na rangi nyeupe isiyo na urembo) jozi mbili (2)

NB: NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUSUKA NYWELE KWA MTINDO WOWOWTE ULE, KUWEKA DAWA (BLICH) KICHWANI, KUTUMIA VIPODOZI VIKALI VINAVYOWEZA KUATHIRI NGOZI YAKE AU KUJA NA NGUO ZOZOTE ZA NYUMBANI.

**4. VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI**

1. Mathematical set
2. Non programable calculator
3. English dictionary
4. Daftari kubwa zisizopungua 09 kwaajili ya nukuu za masomo na daftari zingine 09 za msomi kwaajili ya mazoezi ya darasani
5. Kalamu za wino (peni) na pencil
6. Ream 2 (double A) kwa mwaka kwaajili ya majaribio na mitihani. Ream isiyo double A haitapokelewa
7. Vitabu vya masomo angalau matatu ambavyo vitakua ni mali yake binafsi
8. Begi la mgongoni la kubebea madaftari na vifaa vya kusomea
9. File holder mbili (02) kwaajili ya kuhifadhia nyaraka muhimu na kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi

## 5. MAHITAJI YA BWENI

- Sanduku la chuma (tranka) la kutunzia vifaa vyake binafsi na kufuri imara
- Godoro la futi 3x6
- Shuka mbili za kijani, blanketi, mto na foronya za rangi ya kijani
- Galoni ya lita 5 ya kuhifadhia maji ya kunywa
- Neti nyeupe 4x6
- Magauni mawili (02) marefu ya kushindia (shamba dress) kitambaa cha draft blue na nyeupe mshono wa SOLO (kitambaa Kizito grade 1)
- Trucksuit nzito moja ya darkblue yenye ufito mweupe pembeni na T-shirt au jezi yake ya darkblue yenye kola na fito nyeupe
- Toilet paper za kutosheleza matumizi yake
- Sanitary pads zakutosha (zisipungue pact 5)
- Kiwi nyeusi na brush yake
- Vifaa vya usafi mopper, squizer, chelewa, hard bloom na soft bloom, jembe moja na mpini wake, fyekeo moja na leki moja (**NI LAZIMA**)
- Ndoo ndogo (lita 10) mbili (02) na kopo la kuogea
- Tochi aina  ya D light moja kwaajili ya matumizi wakati umeme unapokatika
- Malapa/ndala za kuogea
- Sabuni ya maji lita mbili (02) kwa ajili ya usafi wa vyoo na bafu bwenini
- Kanga/kitenge jozi moja na taulo moja
- Mafuta ya kujipaka mwilini,sabuni,miswaki na dawa ya meno
- Saa ya mkononi
- Fedha ya matumizi ya mwanafunzi (pocket money)

## 6. HUDUMA ZA CHAKULA

Mwanafunzi aje na vifaa vya chakula (Sahani au container, kikombe na kijiko) atakula chakula kinachoandaliwa shuleni.

## 7. HUDUMA YA AFYA NA MATIBABU

Huduma ya afya na matibabu ni jukumu la mzaza/mlezi wa mwanafunzi. Shule itahusika na huduma ya kwanza tu. Endapo mwanafunzi ana magonjwa ya kudumu mfano pumu(asthma) anashauriwa kuja na dawa anayoitumia au bima ya afya.TUNASISITIZA MWANAFUNZI KUWA NA BIMA YA AFYA. **Kwa wanafunzi ambao hawana bima waje na pesa kiasi cha Tsh 50,400/= kwaajili ya kukatiwa bima**

## 8. SHERIA ZA SHULE

Shule ya sekondari CHIEF SAROTA inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha iazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kuzingatia sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoainishwa

### A. KILA MWANAFUNZI NI LAZIMA AZINGATIE MAMBO YAFUATAYO

- ✓ Heshima kwa watu wote (walimu wafanyakazi ambao sio waalimu viongozi wa shule wanafunzi wengine wazazi na jamii yote kwa ujumla)
- ✓ Kuhudhuria shughuli zote za shule za ndani na nje kulingana na ratiba elekezi ya shule
- ✓ Kuwahi katika shughuli zote za shule
- ✓ Kusaini mkataba wa taaluma shuleni kuhusu kufanya vizuri na kufaulu mitihani yake yote
- ✓ Kutunza mazingira na usafi wa shule wakati wote
- ✓ Kulinda na kutunza mali za shule awapo shuleni
- ✓ Kufuata ratiba ya shule wakati wote,kusoma kwa bidi na kufanya kazi za darasani
- ✓ Kuheshimu tamaduni na taratibu za jamii inayotuzunguka

### B. MAMBO AMBAYO HARUHUSIWI KUFANYA AWAPO SHULENI NA YANAWEZA KUPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Kuvuta sigara, bangi au ulevi wa aina yeyote
ii. Wizi wa aina yeyote
iii. Kuvaa au kumiliki mavazi yasiyo sare za shule ndani ya eneo la shule
iv. kufuga nywele,kusuka ,kufuga kucha kupaka rangi/hina kucha kunyoa mitindo isiyofaa awapo shuleni
v. kupigana au kuchochea ugomvi
vi. Kujihusishwa na mahusiano ya kimapenzi awapo shuleni
vii. kumiliki au kutunza simu au kifaa kinachohusiana na simu (line,charger,memory card au flash)awapo shuleni
viii. kumiliki vifaa ya umeme kama redio,heater au pasi ya umeme awapo shuleni
ix. kutoka nje ya shule bila ruhusa kutoka wa Mwalimu
x. kushiriki au kuchochea migomo shuleni
xi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na makosa ya jinai
xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
xiii. Kutumia lugha matusi kwa walimu,wafanyakazi ambao sio waalimu au wanafunzi wenzake

**HITIMISHO MUHIMU**

Tafadhali soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

1. Hatutopokea fedha taslimu shuleni, hivyo malipo yote ya michango ya shule yafanyike BENKI isipokua malipo ya vifaa vinavyoweza kupatikana shuleni.
2. Mwanao haruhusiwi kuja shuleni na simu ya kiganjani, pasi ya umeme, redio, heater,computer, na Tv. **AKIPATIKANA NA VIFAA HIVI, ADHABU YAKE NI KUONDOLEWA SHULENI PAMOJA NA KULIPIA FIDIA YA UHARIBIFU WA MIUNDOMBINU YA SHULE KIASI KISICHOPUNGUA Tsh. 350,000/=**
3. Haturuhusu mwanafunzi kutembelewa shuleni na watu wasio fahamika.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi sehemu ya kuchukulia chakula mara kengele ya chakula inapogongwa akiwa na vyombo vya chakula
5. Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalum **(special diet)** kwa wale wenye changamoto za kiafya ya kutokula baadhi ya chakula
6. Mwanafunzi atumiwe nauli mapema kabla ya kufunga shule ili utaratibu wa usafiri uweze kuandaliwa mapema
7. Ratiba ya shule huanza saa **11:00 alfajiri** kwa mchakamchaka, kufanya usafi binafsi na usafi wa mazingira
8. Mwanafunzi ataruhusiwa kusali katika dhehebu lake shuleni kulingana na utaratibu uliowekwa na shule
9. Mawasiliano ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yapitie katika uongozi wa shule. **HATURUHUSU MWANAFUNZI KUPIGA SIMU SHULENI, BALI ATATUMIA UTARATIBU WA MAWASILIANO ULIOWEKWA SHULENI.**

**HAKIKISHA MWANAO ANAKUJA NA MAHITAJI YOTE MUHIMU NA ANARIPOTI KWA WAKATI AKIWA NA;**

- ✓ Barua/Fomu hii ya kujiunga shuleni ikiwa imejazwa vyema
- ✓ Bank pay slip original ya malipo ya michango ya shule iliyoainishwa
- ✓ Nakala ya Result slip inayoonyesha matokeo yake ya kidato cha iv
- ✓ Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- ✓ Fedha ya kulipia mahitaji yanayopatikana shuleni kama ilivyoainishwa kwenye fomu hii
- ✓ Vifaa/mahitaji yote muhimu kwa matumizi binafsi/shule
- ✓ Fomu ya hospitali na maelekezo binafsi zijazwe kwa usahihi

**SCHOOL MOTTO: “EMPOWERING MINDS FOR TOMORROW”**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHIEF SAROTA**

**……………………**

**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI CHIEF SAROTA**

**FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi…………………………………………………………………….
2. Anuani ya nyumbani…………………………………………………………………………..
3. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………
4. Mahali ulipozaliwa
   kijiji/mtaa………………………………Kata……………………………………….…….
   Tarafa…………………………Wilaya………………………Mkoa……………………..
5. Mahali unapoishi kwa sasa
   kijiji/mtaa……………………………………Kata……………………………………….
   Tarafa…………………………Wilaya………………………Mkoa……………………..
6. Shule msingi ulikotoka…………………………Anwani……………………………….
7. Dini/Dhehebu……………………………………………………………………………
8. Kabila…………………………………………………………………………………….
9. Taifa (Mtanzania/si mtanzania)…………………………………………………………..…
10. Michezo uipendayo (hobbies)…………………………………………………...…….
11. **JAMAA KATIKA FAMILIA AMBAO WANAWEZA KUPELEKEWA TAARIFA ZAKO MUHIMU KWA MASUALA YAHUSUYO SHULE.**
    **(JAZA SEHEMU ZOTE, PAMOJA NA ANGALAU PASSPORT SIZE YA MZAZI/MLEZI MMOJA)**

i. Jina la Baba…………………….……….Namba ya simu…………………………..
   Kazi yake……………………………………..Anuani………………………………
ii. Jina la Mama…………………...……… Namba za simu…………………………..
   Kazi yake……………………………………Anuani………………………………….
iii. Jina la mlezi……………………….……...... Uhusiano…………………….....
   Namba ya simu………………................... Kazi yake………………………………...
   Anuani……………………………………………

| 1. **PICHA** | 2. **PICHA** | 3. **PICHA** |
|---|---|---|
| | | |

## FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA TARATIBU ZA SHULE

## UTHIBITISHO NA AHADI

Mimi (jina la mwanafunzi)………………………………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa nilizo jaza hapo juu niza kweli, nakubali kwa dhati nafasi niliyopewa na taifa ya kujiunga na shule ya Chief Sarota Sekondari. Naahidi kufuata sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule. Naahidi kutokua mkaidi au mtovu wa nidhamu na nitatumia vizuri nafasi hii kusoma kwa bidii, kujipatia maarifa yatakayonisaidia mimi mwenyewe, jamii na taifa langu.

EE MWENYEZI MUNGU NISAIDIE!

Sahihi ya mwanafunzi……………………………… Tarehe ……………………..…

Mimi (jina la mzazi/mlezi wa mwanafuzi)………………………………………………ambae ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………..…………………………………..nimeyasoma masharti na sharia za shule ya sekondari Chief Sarota ambako kijana/binti yangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kusoma kwa bidii na kufuata sharia, kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa na zitakavyoelezwa. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule kama malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa taifa letu.

Endapo nitashindwa kutimiza majukumu yangu ya kumlipia mwanangu ada na michango halali ya shule kwa wakati, nipo tayari kuwajibishwa ikiwa ni pamoja na kufikishwa katika vyombo vya sharia kwani kufanya hivyo ni kuhatarisha maendeleo ya mwanangu na mipango na mikakati ya shule kwa ujumla.

………………… …………………

Sahihi ya mzazi Tarehe

**ASANTE KWA USHIRIKIANO**

**SHULE YA SEKONDARI CHIEF SAROTA**

**FOMU YA AFYA YA MWANAFUNZI (MEDICAL EXAMINATION FORM)**

**IJAZWE NA MGANGA WA HOSPITALI YA SERIKALI AU KITUO CHA AFYA CHA SERIKALI TU!**

Kumb. Na.KSS/MEDICAL/F.V Tarehe …………………………

Mganga Hospitali/Kituo cha afya.………………………………S.L.P …………………………

Jina la mwanafunzi…………………………………………………………………………….

**YAH: KUPIMA HALI YA AFYA YA MWANAFUNZI**

Shule ya Sekondari Chief Sarota inakuomba kupima na kujaza taarifa ya afya ya mwanafunzi tajwa hapo juu kabla ya kujiunga na masomo ya kidato cha tano (V)

I. MACHO (VISION) ………………………………………………………………..
II. KIFUA KIKUU (TB) ………………………………………………………………
III. PUMU (ASTHMA)…………………………………………………………………
IV. SHINIKIZO LA DAMU (BP) …………………………..………………………...
V. KISUKARI (DIABETES) ………………………………………………………...
VI. MAGONJWA YA ZINAA (VENERAL DISEASE) …………………………………..
VII. MATATIZO YA USIKIVU (HEARING IMPAREMENT) ……………………………
VIII. MALARIA SUGU ………………...……………………………………………..…….
IX. ULEMAVU WA VIUNGO (PHYSICAL DISABILITIES) Taja ……………………
X. MIMBA …………………………………………………..……………………
XI. MATATIZO YA AKILI ……………………………………………………………
XII. MATATIZO YA MOYO ……………………………………………………………
XIII. MATATIZO YA TUMBO …………………………………………………………..
XIV. DAMU (BLOOD EXAMINATION) ………………………………………………..
XV. DAMU (BLOOD GROUP) …………………………………………………………..
XVI. KUSUMBULIWA NA KICHWA (HEADACHE) ……………………………………..
XVII. KICHOCHO ……………………………………………………………………...
XVIII. MARADHI MENGINE ……………………………………………………………

NB: Endapo kuna maradhi yamebainika kwa mwanafunzi apatiwe matibabu kabla ya kuripoti shule.

Nimemfanyia vipimo mwanafunzi tajwa hapo juu na ninathibitisha kwamba afya yake ni njema/si njema kuendelea na masomo ya kidato cha tano.

Jina la mpimaji ……………………………………Sahihi …………………………………

Cheo……………………………………. Tarehe …………………………………..

## REFERENCE BOOKS

**Geography**

1. Physical Geography – TIE
2. Practical Geography – TIE
3. Physical Geography - MSABILA

**Chemistry**

1. General and Inorganic chemistry –TIE
2. Physical chemistry–TIE
3. Organic Chemistry – TIE
4. S. Chand’s Principles of Chemistry – XI & XII

**Biology**


1. Biology for secondary schools form five - TIE
2. Biology for secondary schools form six – TIE
3. Biological science – Oxford

## REFERENCE UNIFORMS


**Track suit**



**Neck tie**



**Shamba dress**



**Jezi**



**Sketi ya shule**



**Sweta**

